BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Nne – Tarehe 25 Mei, 2016.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Hotuba ya Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2013/2014, Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2013/2014, Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu ya Mfuko wa Barabara kwa Mwaka 2013//2014 na Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) 2011/2015.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC):

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC) kuhusiana na Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2013/2014, Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2013/2014, Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu ya Mfuko wa Barabara kwa Mwaka 2013//2014 na Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) 2011/2015.

II. MASWALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:

34. MHESHEMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kupewa majukumu ya kufungua kesi na kusimamia kazi ambayo ilikuwa ikifanywa na Jeshi la Polisi.

a) Kwa nini kumekuwepo na ucheleweshaji mkubwa wa kesi kusikilizwa kwa wakati kutokana na kutokamilika kwa ushahidi na wananchi kulazimika kushuka na kupanda katika majengo ya Mahakama.

b) Uamuzi wa Ofisi ya DPP kupewa kazi ya kufungua na kusimamia kesi kumeleta tija gani kama kesi zinaendelea kuchelewa kutolewa hukumu kati ya miaka 2 na miaka 5.

c) Ucheleweshaji wa kesi unazingatia vipi misingi ya Utawala Bora, wakati Serikali ya Awamu ya (7) inaendeleza mwelekeo wake wa kuimarisha Utawala Bora Zanzibar.

WAZIRI WA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI:

84. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kwa kuwa Kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu na ardhi yetu ya Zanzibar imekua ikikubali mazao ya muda mfupi kama vile mpunga, muhogo na migomba. Na kwakuwa baadhi ya wananchi wamekuwa wakimiliki maeneo makubwa bila ya kuyatumia,

Kwa nini Serikali isiyatumie mashamba hayo kwa kuyalima mazao ya muda mfupi mpaka pale wamiliki wake watakapokuwa tayari kuyatumia.

WAZIRI WA HABARI, UTALII, UTAMADUNI NA MICHEZO:

54. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika moja ya ziara zake Kisiwani Pemba alifanya ziara katika uwanja wa Gombani na kukagua vifaa mbali mbali vya ujenzi wa tatani kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya mchezo wa mbio za riadha. Kwa kuwa uwanja wa Gombani ulikuwa unategemea kumaliza matengenezo hayo katika Sherehe za Mapinduzi za mwaka 2016 lakini mpaka leo bado.

a) Je, ni tatizo gani linalokwamisha kumaliza matengenezo ya uwanja huo.

b) Ni Kampuni gani inayotengeneza tatani za Uwanja huo na chini ya mtaalamu gani.

WAZIRI WA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI:

11. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Serikali inastahiki pongezi kwa kujengwa barabara ya Kenya Chambani ambapo hatua kubwa imefikiwa lakini barabara hii imefika Ukutini kwa Mtora tu na haikufika Matele na Chwale na pia barabara hii ina milima, kona, na ni nyembamba. Na kwa kuwa maeneo ya Wambaa kwa Azani mpaka Hoteli Kutukuu hawana bararaba mbapo kutoka Kenya Chambani imekuwa kero kwa wanaokwenda kwa miguu na vyombo vidogo vidogo, kwa sababu ina magari mengi na makubwa.

Je, Serikali itasaidia vipi wananchi wa Jimbo la Chambani ili kuondokana na shida hiyo ya usafiri.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwamba Baraza hili lifikirie na kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2016/2017.

IV. KAULI YA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Hotuba ya Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2013/2014, Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2013/2014, Ripoti ya Ukagu`zi Yakinifu ya Mfuko wa Barabara kwa Mwaka 2013//2014 na Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) 2011/2015.

Zanzibar,
25 Mei, 2016.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA